# Tija za Tohara kwa Jamii za Kiafrika: Uchunguzi wa Mhusika Omolo katika Riwaya ya *Ua la Faraja* (2004)

**Adria Fuluge & Martina Duwe**
*Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-05-04
Kurekebishwa: 2025-11-02
Kukubaliwa: 2025-11-08
Kuchapishwa: 2025-11-09

**Maneno Muhimu**
Afrika
Fasihi
Jamii
Tohara

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Fuluge, A., & Duwe, M. (2025). Tija za Tohara kwa Jamii za Kiafrika: Uchunguzi wa Mhusika Omolo katika Riwaya ya *Ua la Faraja* (2004). *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 3*(2), 66-75.

Copyright © 2025

**Ikisiri**
Katika jamii nyingi za Kiafrika, tohara ni mchakato wenye thamani na tija kubwa kwa baadhi ya makabila, husuani kwa kijana wa kiume. Katika makabila hayo, asiyetahiriwa huonekana kuwa bado ni mtoto na hajakomaa kifikra na kiutu, ambapo huweza hata kutengwa katika kushirikishwa baadhi ya masuala ya kijamii. Kijana huyo kama umri wake ni mkubwa, huweza kudharauliwa na rika lake na hata waliopo chini yake. Sambamba na hilo, katika maisha halisi ya Waafrika, tohara huchukuliwa kwa thamani inayoweza kuendeleza na kuhifadhi utambulisho wa kitamaduni na kijamii. Kwao, tohara humfanya mtu atambulike kwa namna tofauti na ilivyokuwa awali. Kwa jumla, thamani ya tohara kwa Waafrika ni suala lililowashughulisha wataalamu wengi. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa tafiti nyingi kuhusu tohara kwa Waafrika, bado tija za tohara kwa kufungamanisha na fasihi andishi haijamakinikiwa kwa umahususi wake. Kwa hiyo, makala hii inashughulikia jambo hilo kwa kumrejelea mhusika Omolo kutoka riwaya ya *Ua la Faraja* (2004). Data za matokeo haya zilipatikana maktabani kwa kutumia mbinu ya usomaji matini. Vilevile, misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi imetumika katika mchakato wa kuchunguza, kuchanganua, na kuwasilisha data zilizozaa matokeo hayo. Mjadala unaonesha kwamba tohara katika maisha ya Waafrika ina tija mbalimbali kulingana na utoshelevu wa kaida zao. Makala hii inajadili tija nne; nazo ni: Kudumisha mila, kuleta heshima kwa mhusika, kujikinga na magonjwa, na kujenga ujasiri na ukakamavu.

## Utangulizi

Waafrika huenzi na kuendeleza mila mbalimbali zinazosawiri maisha yao halisi. Miongoni mwa mila hizo ni tohara. Tohora ni kitendo cha kutahiriwa, kutiwa jando (BAKITA, 2017). Mila hii ni kongwe katika maisha ya jamii nyingi za Waafrika ikiwa na maana pana ya kitamaduni, kijamii, kiuchumi, na hata kidini. Mchakato wa kuendeleza tohara huhusisha maandalizi ya kifikra, kiuchumi, na kijamii (Simiyu, 2007). Kifikra, vijana hurithishwa thamani ya tohara tangu wakiwa wadogo na wanapofikia umri fulani hutambua kwamba lazima wapitie hatua hiyo ili ukamilifu wao wa kimaumbile na kitamaduni uweze kutimia. Kiuchumi, tohara huambatana na sherehe zinazohusu matumizi ya rasilimali kama vile mifugo, fedha, na nafaka. Kijamii, tohara kwa Waafrika huambatana na sherehe zinazopangwa kimatukio kulingana na kaida za jamii husika. Masuala kama vile, uchezaji wa ngoma, ulaji, na unywaji hupewa kipaumbele katika kutimiza shughuli hiyo. Nyimbo huandaliwa kulingana na mafunzo yanayolengwa kutolewa kwa wakati husika (Mutwiri, 2005). Mchakato wa tohara unahusisha upasuaji wa sehemu za siri kwa wavulana na wasichana kwa sababu za kitamaduni, kijamii, au kidini. Kwa upande wa wavulana, tohora mara

nyingi hutekelezwa kama sehemu ya mchakato wa ubalehe au maandalizi ya kuwa mtu mzima mwenye uwezo wa kuimiliki familia. Mafunzo yanayotolewa huwa kielelezo cha usafi, ujasiri, ukakamavu, na utii kulingana na kaida zao (Nandwa, 1976). Katika muktadha huu, tohara huambatana na mafundisho ya maadili, wajibu wa kifamilia, na heshima kwa jamii. Aidha, tohara hujenga mshikamano wa kijamii kwa kuwaunganisha vijana waliotahiriwa kama kundi muhimu lenye majukumu na thamani mpya.

Asili ya tohara inayofanywa katika jamii nyingi za Kiafrika imejinasibisha na misingi ya tamaduni zao. Kabla ya kuingiliana na mataifa ya kigeni kama vile, Wazungu na Waarabu, Afrika ilikuwa na mila ya tohara iliyoendeshwa kwa kizingatia kaida zao. Mathalani, huko Misri, tohara ilichukuliwa kama msingi wa kumwandaa kijana wa kiume kuingia katika utu uzima (Dunsmuir & Gordon, 1999). Tangu kale, tohara ililenga kurithisha maarifa ya usafi, heshima, uwajibika, na utambulisho wa rika fulani ambalo hupokea mabadiliko ya kimajukumu na kijamii. Mbiti, (1969) anaeleza kwamba kwa upande wa Afrika Mashariki, baadhi ya jamii zilizokuwa zinathamini na kuendeleza tohara ni Wamasai, Wagisu, na Wakamba. Anaendelea kueleza kuwa baadhi ya jamii za Kiafrika huamini kwamba kufanyiwa tohora ni jambo linalokinzana na mapenzi ya Mwenyezi Mungu katika uumbaji wake. Hivyo, kwao tohara siyo suala la muhimu. Uislamu au Ukristo uliendeleza mila ya tohara, hasa kwa wanaume kwa kuwa mila hiyo inafungamana na misingi ya maandiko ya dini hizo. Hata hivyo, kwa wasichana, mara tohora nyingi huchukua sura ya ukeketaji, kitendo kinachopingwa vikali na mashirika ya afya duniani, kama vile WHO, kutokana na madhara yake kiafya, kisaikolojia, na kijinsia (WHO & UNAIDS, 2007). Katika karne ya 21, changamoto kuu zinazojitokeza ni mvutano kati ya kuhifadhi utamaduni na kulinda haki za binadamu, hususani kwa wanawake na watoto. Jamii nyingi za Kiafrika zimeanza kuchukua hatua za kisheria kuzuia tohara kwa wanawake (ukeketaji) huku zikiruhusu au kusimamia tohara kwa wavulana kwa njia salama ambazo huzingatia kanuni za kiafya (Kanake, 2001).

Pamoja na ukosoaji dhidi ya mila hii, hasa inapotekelezwa kwa wasichana, kwa kuangazia madhara ya kimwili, kisaikolojia, na kijinsia yanayotokana na ukeketaji, bado baadhi ya jamii za Kiafrika hazijaiacha mila hii, hususani kwa vijana wa kiume (WHO & UNAIDS, 2007). Hivyo, tohara imepewa nafasi ya kipekee kama mojawapo ya mada zinazojadiliwa kwa kina kwa lengo la kuibua tafakuri kuhusu maana yake, athari zake, na nafasi yake katika muktadha wa kale na wa sasa. Kwa minajili ya makala hii, tohara inayomakinikiwa ni ile inayotekelezwa kwa mwanamume kwa kuzingatia misingi ya maisha halisi ya Waafrika. Kwao, mchakato huo una tija ya kueneza na kuendeleza maadili kulingana na kaida zao. Hii inatokana na ukweli kwamba mafunzo yanayotolewa wakati wa tohara, huakisi maisha halisi ya jamii na hulenga kuendeleza maarifa ya kimaadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa kuzingatia hilo, sanaa, hususani fasihi andishi hutumika kubainisha maarifa hayo kwa kuelimisha, kuasa, kuhoji, na kubadilisha mitazamo ya jamii kuhusu tohara. Kwa kutumia lugha ya kisanaa, wahusika, na mandhari, huchochea mijadala ya kina kuhusu mila na desturi za Waafrika. Wahusika wa kifasihi husawiriwa kisanaa na msanii ili kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha ya mwanadamu kulingana na utamaduni wa jamii (Msokile, 1992; Duwe, 2023). Katika muktadha huu, fasihi inakuwa kiwakilishi cha sauti za waliotahiriwa, wanaotetea na kupinga mila hiyo, na jamii kwa ujumla katika safari ya kuelekea mabadiliko ya kijamii (Simiyu, 2007). Kwa msingi huo, katika mazingira halisi ya Waafrika, sanaa, ikiwemo fasihi imekuwa nguzo muhimu ya kulinda, kuhalalisha, na kuhimiza jamii kuthamini tohara kama nyenzo muhimu ya kubainisha ukamilifu na utu wa mwanamume katika jamii yake.

**Muhtasari wa Sifa za Mhusika Omolo**

Mhusika Omolo ni miongoni mwa wahusika wakuu katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2004). Uhusika wake unaweza kumulikwa na kufafanuliwa kulingana na sifa bainifu zinazomtambulisha na kumtofautisha na wahusika wengine. Mhusika huyu amebeba sifa ya kuutetea na kuukumbatia ujadi uliofichwa katika misingi ya unyenyekevu, utii, ukarimu, na huruma. Vilevile, amebeba sifa ya uchapakazi inayomfanya apendwe na kila anayekwenda kupata huduma katika ofisi yake. Sambamba na hayo, mwandishi amefanikiwa kumchora Omolo kama kiwakilishi cha jamii zisizojua tija za tohara katika muktadha wa kiafya na kijamii. Omolo anaonekana ni mwenye kutunza mila na desturi za jamii yake ikiwamo kupinga tohara ili kundeleza utamaduni wao. Pamoja na usomi wake, anaichukulia tohara kama mapinduzi ya kifikra yanayokinzana na lengo la Mungu katika kumuumba mwanadamu. Hii ni athari ya kimalezi ambapo katika jamii iliyomkuza, tohara kwa kijana wa kiume ni kinyume na utamaduni wao. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kiwakati na mwingiliano wa kijamii, inamlazimu Omolo kukubaliana na suala la kufanyiwa tohara katika umri mkubwa. Jambo hilo linaongeza kujiamini kwake, kuwa huru, na kujiona ni sehemu ya jamii halisi ya sasa. Kupitia mhusika huyu na wengine, mwandishi anaiasa jamii kuwa maisha ya starehe husababisha kuenea kwa magonjwa yanayoambukiza. Pia, anadokeza athari za UKIMWI kwamba hurudisha nyuma maendeleo ya familia na jamii na husababisha sonona na vifo katika mnyororo wa kimahusiano ya kifamilia. Vilevile, anahitaji jamii ijikomboe kifikra juu ya magonjwa, hususani yanayotokana na ngono, ambapo kutofanyiwa tohara ni sababu mojawapo ya kuenea kwa magonjwa hayo. Kwa kuzingatia hilo, mjadala huu umemakinikia jambo hilo kwa kubainisha tija za tohara kwa kumrejelea mhusika Omolo pekee.

**Mwegamo wa Nadharia**

Makala hii ni zao la utafiti uliofanyika kwa kujiegemeza katika misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi. Inaelezwa na Coser (1963) kwamba waasisi wa nadharia hii ni Charles Taylor (1822-1917) pamoja na George Lukacs (1885-1971). Wataalamu hawa wanaitazama sanaa, hususani fasihi kama zao linalohusisha mipaka ya kijiografia, kiutamaduni, na mazingira ya jamii husika. Kwa msingi huo, kila jamii imefungwa kwa mipaka fulani ambayo huweza kuwa tofauti na jamii nyingine. Kutokana na hilo, Wanasosholojia ya Kifasihi wanadai kwamba fasihi inatakiwa iakisi na kutoa taarifa za kweli kuhusu maisha halisi ya jamii. Msingi wa hoja hiyo ni kwamba, nadharia hii huangazia na kubainisha uhusiano uliopo baina ya kazi ya kifasihi na maisha halisi ya jamii iliyoiunda kazi hiyo. Vilevile, huonesha na hufafanua sababu za kutokea, kuibuka, na kutendeka kwa kazi ya fasihi yenye sura na umbo la kijamii na namna mtazamo wa msanii wa kazi hiyo, unavyoongozwa na utamaduni na maisha halisi ya jamii husika. Msisitizo wa Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi umejikita katika kutazama namna kazi ya sanaa, hususani fasihi inavyohusiana na maisha halisi ya jamii husika. Hii ni kwa kuwa fasihi na mazingira ya jamii yenye kuhifadhi mila na desturi zao, haviwezi kutenganishwa (Glicksberg, 1972). Kwa kuzingatia hilo, katika uhakiki wa kazi za kifasihi, msanii anapaswa kuhusisha vema uhusiano wa vipengele vyake muhimu, yaani fani na maudhui ili uumane na uhalisi wa mazingira ya jamii husika. Suala hili limezingatiwa vema na watafiti wa makala hii, ambapo nadharia hii imekuwa nguzo muhimu katika kuchunguza, kuchanganua, na kuwasilisha data zinazohusu tija za tohara kwa jamii kwa kumrejelea mhusika Omolo kutoka riwaya ya *Ua la Faraja* (2024).

**Methodolojia ya Utafiti**

Makala hii inatokana na utafiti uliofanyika kwa mwegamo wa kitaamuli. Mwegamo huu umejikita katika kuhusisha taarifa za kimaelezo wakati wa ukusanyaji wa data, uchanganuzi, na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Kwa jumla, uchunguzi uliotoa data za matokeo haya ulifanyika maktabani, ambapo watafiti walizisoma nyaraka mbalimbali zilizotoa maarifa yaliyojadiliwa katika makala hii.

Riwaya ya *Ua la Faraja* (2004) iliteuliwa kama nyaraka ya msingi katika kuchunguza tija za tohara kwa jamii za Kiafrika kwa kumrejelea mhusika Omolo. Uteuzi wa mhusika huyu umezingatia kigezo kwamba ni mhusika mkuu aliyevikwa uhusika wa kuziishi, kuzikumbatia, na kuendeleza mila za jamii yake, ikiwamo mila ya kutoondoa govi katika uume wake. Hata hivyo, mhusika huyo baadaye anatambua tija za tohara kwa mwanaume na kukubaliana na ushauri wa kufanyiwa tohara.

**Tija za Tohara**

Katika jamii nyingi za Kiafrika, tija za tohara huweza kufafanuliwa kwa namna tofautitofauti. Makala hii inajadili tija nne; ambazo ni: kudumisha mila, kuleta heshima kwa mhusika, kujikinga na magonjwa, na kujenga ujasiri na ukakamavu.

**Kudumisha Mila**

Mila ni taratibu za kimaisha za mwenendo na jinsi ya kufanya mambo zinazofuatwa na jamii fulani kulingana na historia na utamaduni wao (BAKITA, 2017). Mingoni mwa masuala yanayotambulisha mila za jamii ni tohara, ambayo humulikwa kama utambulisho wa kijamii na kitamaduni. Mbiti (1969) anaiona tohara kama sehemu ya mzunguko wa maisha, ambapo kijana hupitia hatua ya mpito kutoka utoto hadi utu uzima kwa kufuata mila na desturi za jamii husika. Hii ina maana kwamba mhusika anapopitishwa katika hatua hizo, hupata maarifa ya kudumisha mila za jamii yake, ambapo naye, huendelea kuyarithisha kwa vizazi vingine. Hivi ndivyo anavyoeleza mwandishi wa riwaya ya *Ua la Faraja* kwamba, kila jamii inapaswa kuzingatia mila zake na kwamba jamii inayopuuza mila hizo, ni sawa na mtumwa. Anamtumia mhusika Omolo kama kiwakilishi cha wale wasiopenda kutimiza mila ya tohara. Mwandishi kupitia sauti ya Dkt. Hans anasema:

> Katika maongezi yake, Dkt. Hans alikazania maoni yake kuhusu jando na athari za Waafrika kutelekeza mila zao. "Msahau kwao ni mtumwa," Dkt. Hans alisisitiza. Akaeleza kwamba Waafrika sasa wamekuwa watumwa wa mila na tamaduni za wenzao, kuanzia imani hadi uchumi na siasa. Alidai kwamba Mwafrika amezoea kutofanya jambo lolote sharti kwanza ajipime kwa Mzungu au Mwarabu. Leo hii sijui Msukuma wa asili aliamini nini. Hata asili ya kizazi chetu imesahaulika. Ona upuuzi huo: watu wamedanganywa na Wazungu mpaka wakasahau umuhimu wa historia na asili yao! Hata mila ya jando ambayo hugusia kuhusu historia ya kabila letu imebaki tohara tu, na kufundisha uhodari wa ngono (uk. 357 - 358).

Katika dondoo hilo, mwandishi anaonesha namna jamii za Kiafrika zinavyotakiwa kuzingatia na kuendeleza mila zao. Anasikitishwa na wale wanaoziacha mila hizo na kuwa watumwa wa mila na tamaduni za kigeni. Msisitizo wake ni kwamba mila hizo likiwamo suala la tohara, ni muhimu kwani huhifadhi historia ya jamii husika. Suala hili linaungwa mkono na Nandwa (1976) anaposema kuwa tohara ilikuwa kati ya shughuli muhimu sana kwa mja binafsi na jamii husika; kwani watahiriwa walipewa maadili mema, utu uzima, siri, utamaduni, na historia ya jamii. Akielezea umuhimu wa tohara kwa jamii ya Wabukusu, Manguliechi (2007) anaona kwamba tohara katika jamii hiyo ina umuhimu mkubwa na inathaminiwa kwa muda mrefu. Anafafanua zaidi kwamba tohara huambatana na nyimbo za nyiso, ambazo hubeba dhima mbalimbali kama vile kuonya, kuadilisha, kukashifu, kuburudisha, na kuelimisha. Kwa kuzingatia mtazamo wa Wanasosholojia ya Kifasihi kuwa sanaa lazima isawiri mazingira na utamaduni wa jamii, suala hili ni halisi katika jamii nyingi za Kiafrika, kwani hufanya tohara kwa watoto wa kiume na hata watu wazima, ambao hawakufanikiwa kufanyiwa tohara katika umri wao wa utoto, ili kutunza thamani na utu wao.

**Kuleta Heshima kwa Mhusika**

Katika jamii, kila mtu anastahili kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wake. Heshima ni thamani anayopewa mtu machoni mwa jamii yake (BAKITA, 2017). Yapo mambo mengi yanayoweza kumfanya mtu apate heshima anayostahili na kuthaminiwa utu wake katika jamii, likiwamo suala la tohara. Kwa mfano, ikiwa katika jamii suala la tohara linapewa umuhimu, na akatokea mtu akashindwa kuitimiza jadi hiyo; mtu huyo hupoteza heshima na thamani yake katika jamii yake. Mwandishi wa riwaya teule anathibitisha hilo kupitia kwa mhusika, Mima, mwenye kiu ya kufanya mapenzi na Omolo, lakini kiu hiyo inamwishia ghafla, baada ya kubaini kwamba, Omolo hajafanyiwa tohara. Hili linathibitishwa na mwandishi kupitia majadiliano baina yao kama ifuatavyo:

> "Nitapiga kelele kuita watu," Mima alimwonya. Kigugumizi cha Omolo kikaondoka.
> "Umeletwa na nani hapa?" Omolo alimuuliza.
> "Nilikuwa nakutaka. Nilivutiwa nawe tufanye mapenzi."
> "Sasa?"
> "Sasa haiwezekani. Ukitaka nenda ukakate."
> "Nikakate nini?"
> "Zunga."
> "Zunga ndiyo nini?" Omolo aliuliza.
> Mima akacheka. Omolo akazidi kughadhabika. Mima akasema kwa sauti ya kunong'ona, "Katahiriwe." (uk. 28 – 29).

Nukuu hiyo inatupa picha kwamba Omolo amepoteza heshima na utu wake kwa Mima kwa sababu hajafanyiwa tohara. Hata pale anapoonesha kushikwa na hamu ya kutaka kufanya mapenzi kwa kumlazimisha Mima ampe anachokitaka, Mima anamtisha kwamba atapiga kelele. Anachomshauri ni kwenda kufanyiwa tohara ili apate heshima katika jamii na kuweza kufanya mapenzi kwa uhuru na furaha. Naye, Gennep (1977), wanaeleza kwamba tohara humbadilisha mvulana kuwa mume, mwoga kuwa shujaa, na inampa mvulana ruhusa ya kutongoza mwanamke, kumposa, kumwoa, na kumzalisha. Pia, inampa uwezo wa kumiliki mali, kufanya maamuzi ya kibinafsi na kumfungulia njia ya kushiriki katika sherehe zote katika jamii. Hii inatokana na ukweli kwamba tohara huvunja mahusiano ya kitoto na kuunda mambo mapya ya kiutu uzima kimtazamo, kitamaduni, na kijamii.

Kwa upande wa Omolo tohara inaonekana kama kitu kisicho na thamani kwake, kwani hata anaposhauriwa na Mima kwamba akatahiriwe, yeye anadadisi iwapo anayemshauri amefanyiwa jambo hilo ama la! huku akiuliza tija za tohara kwa kuhamaki. Mwandishi kupitia wahusika hawa anasema:

> "Wewe umetahiriwa?" Omolo alimuuliza Mima.
> "Tohara ya wanawake imekatazwa," Mima alimjibu.
> "Na ya wanaume ina umuhimu gani?"
> "Zunga siyo zuri, hata Mungu alimshauri Ibrahimu kutahiriwa na kuwatahiri wanawe."
> "Kwa nini asikate hayo mazunga hukohuko mbinguni?"
> "Hayo mimi siyajui, ila naona kinyaa kufanya mapenzi na mtu mwenye hili!" (uk. 29).

Pamoja na mambo mengine yanayojitokeza katika majadiliano yao, mwandishi anaonesha kwamba tohara huweza kumvutia na kumfurahisha mtu wakati wa kufanya tendo la ndoa. Mima anaeleza kwamba hawezi kufanya mapenzi na mtu mwenye zunga kwa sababu anaona kinyaa. Ifahamike kwamba Mima ndiye akiyemfuata Omolo na kumtaka wafanye mapenzi, lakini kitendo cha Omolo

kutotahiriwa kinamfanya aishiwe hamu ya kufanya naye ngono. Badala yake anaamua kuvaa nguo zake, huku akimwacha Omolo akiwa na uchu wa kufanya ngono. Kitendo hicho kilimfanya Omolo ajione kama amedharauliwa na Mima kwa kuvunjiwa heshima yake. Kwa kujikita katika mawazo ya Wanasosholojia ya Kifasihi, kwamba fasihi hudokeza na kuwasilisha yanayotokea katika jami husika, jambo hili ni halisi katika suala la mahusiano. Kijana, anayeishi na govi hawezi kuthaminiwa, hasa katika muktadha wa kufanya ngono.

Vilevile, matokeo yanaonesha kwamba Omolo anadharauliwa na Queen baada ya kubaini kwamba hajatahiriwa. Hili linathibitika pale ambapo Queen anataka kufanya ngono na Omolo, lakini anashangazwa kuona kwamba Omolo ana govi. Kitendo hicho kinamfanya aishiwe nguvu na hamu ya kufanya ngono. Hata hivyo, huyu anakuwa na uvumilivu kwani anakubali kufanya naye ngono kwa sharti la kutumia mpira (kondomu). Bila shaka naye anaona kinyaa kama ilivyo kwa Mima. Ndiyo maana, baada ya kufanya tendo hilo, Queen anamshauri Omolo akakate zunga lake ili wasiendelee kutumia mipira wanapokutana kingono. Mwandishi anathibitisha kwamba:

> Kama Mima siku ile, Queen alishitushwa na kutotahiriwa kwa Omolo. Lakini yeye akawa mstaarabu. Hakucheka wala kughairi. Ila alikwenda kabatini, akatoa mpira wa kiume, akamvalisha. Na siku ile ikawa ya kwanza kwa Omolo kulifurahia tendo lile akiwa katika utu uzima wake. Mipira miwili ilitumika siku ile aliporudi nyumbani kwake ilikuwa usiku. Alichoka sana. Hakuwa na hamu ya kwenda *Malaika Bar*. Kama siku ile ya kwanza, walitumia mipira. Queen akamwambia, "Bwana ukate hilo zunga lako. Mambo ya kutumia mipira kila siku hayapendezi." (uk. 61 - 62).

Kitendo cha Queen kushangaa anapomwona Omolo akiwa hajafanyiwa tohara, kinatupa picha kwamba tohara ni suala linalofahamika na la muhimu katika jamii. Pia, mwandishi anaposema kwamba hakucheka wala kughairi anaonesha kwamba kutofanyiwa tohara ni kinyume na mila za jamii yake. Hata hivyo, mwandishi haoneshi bayana kama Omolo aliridhia au alilazimishwa kuvalishwa mpira na kufanya ngono kwa hiari yake, licha ya kuwa na uhitaji wa kimwili. Kwa hiyo, Omolo kuwa na govi ni kitendo kilichomwondolea heshima mbele ya Queen.

Matokeo yanaonesha kwamba Queen anapomshauri Omolo akakate zunga lake, anakusudia kuonesha kwamba anastahili kubeba majukumu ya kiutu uzima likiwamo suala la kufanya ngono na kulifurahia tendo hilo. Hata hivyo, Omolo anaonesha msimamo tofauti kuhusu thamani ya ngono katika maisha yake. Mwandishi anathibitisha hilo kupitia majadiliano baina ya Omolo na Dkt. Hans kama ifuatavyo:

> "… siihitaji furaha ya ndoa," Omolo alisema kwa msisitizo na kuonyesha kwamba amechoshwa na maongezi yale.
>
> "Na furaha ya ngono pia huihitaji?" Dkt. Hans aliuliza kwa utani.
>
> Omolo akaanza kukasirika. Dkt. Hans akaongeza, "Unaichukia, au siyo? Unaichukia ngono. Basi ujue ngono ni wajibu wako! Ngono ndiyo nyenzo pekee ya kuzaa, na kuzaa ni wajibu. Usipozaa unaisaliti mbegu ya kizazi kilichoishia kwako. Kila mtu ana wajibu wa kuzaa. Kuoa pia ni wajibu, na kuolewa pia. Ndoa ndiyo asasi ya kukuzia mbegu tunazowajibika kuzizaa. Ni bora kukaribisha furaha katika wajibu na katika asasi hiyo. Ni heri kukaribisha furaha katika wajibu wa ngono na wajibu wa ndoa ili wajibu wa kuzaa na kulea usiwe mzigo …" (uk. 346 - 347).

Nukuu hii inathibitisha kwamba sababu mojawapo ya kumfanyia mtu tohara kwa Waafrika ni kumpitisha katika maisha ya utotoni na kuingia katika daraja lingine kubwa na tofauti la kimaisha. Maelezo hayo yanaungwa mkono na, Mbiti (1969) anafafanua kwamba tohara humpa kijana wa kiume haki na majukumu kama vile, kuoa na kuwa na watoto, kupigania nchi, kushiriki katika sherehe za kifamilia na kurithi mali. Naye, Eliud na wenzake, (2002) wanaeleza kwamba tangu kale tohara ilikuwa ndiyo njia ya kipekee ambayo ilitumiwa kumpitisha kijana kutoka hali ya ujana hadi hali ya mtu mzima. Hivi ndivyo Dkt. Hans anavyomkumbusha Omolo kwamba anapaswa kufurahia ngono kwa kuwa kutokana na tendo hilo, ndipo mtu huweza kutimiza wajibu wake wa kuzaa. Aidha, mtu hupata heshima na utu anapotimiza jukumu hilo la kuzaa na kulea vema watoto wake (Fuluge, 2021). Mtazamo wa Dkt. Hans ni kwamba kama mtu hajafanyiwa tohara, hawezi kuifurahia ngono, kwani hata wanawake wengi huwa na kinyaa kufanya ngono na mtu ambaye hajafanyiwa tohara. Athari yake kubwa ni kwamba mhusika hata akiwa na haja ya kufanya ngono hushikwa na soni, kisha huogopa kutongoza wanawake. Wakati mwingne jamii nayo humtazama kama mwenye upungufu fulani katika viungo vyake vya mwili. Kwa kujiegemeza katika fikra za Wanasosholojia ya Kifasihi kwamba, fasihi ni zao la mipaka ya kitamaduni, ni dhahiri kwamba kitendo cha Omolo kupinga tohara ni athari ya utamaduni wa jamii iliyomkuza.

**Kujikinga na Magonjwa**

Matokeo yanaonesha kuwa kitendo cha Omolo kuishi na govi na kutokuwa tayari kutahiriwa kilimweka katika hatari ya kuambukizwa magojwa mbalimbali, yakiwemo kaswende, kisonono, na UKIMWI. Auvert na wenzake (2005) na Gray na wenzake (2007) wanaeleza kwamba tohara inaweza kupunguza uwezekano wa maambukizi ya magonjwa ya zinaa, kuongeza usafi wa mwili, na kuondoa harufu zisizofaa katika sehemu za siri, hivyo kutoa mazingira salama ya kufanya ngono. Pia, huongeza hali ya kujiamini, jambo ambalo kisaikolojia huchangia mhusika kushiriki tendo la ngono bila hofu wala wasiwasi. Msingi wa hoja hii ni kwamba mtu akifanyiwa tohara ngozi ya kichwa cha uume wake huwa ngumu na huweza kuzuia mtu huyo kupata michubuko kiurahisi, hususani anapofanya ngono, tofauti na mtu ambaye hajafanyiwa tohara (WHO & UNAIDS, 2007). Hii hupunguza hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa mbalimbali yanayohusiana na afya ya uzazi na magonjwa mengine ya zinaa. Mwandishi anathibitisha haya kwa kusema:

> Kasi ya kuenea kwa ugonjwa ule katika jiji la Dar es Salaam ilikuwa kubwa kuliko miji mingine. Wananadharia wengine walitoa sababu za kiuchumi na kisiasa. Dkt. Hans aliamini sababu za kiutamaduni zilichangia zaidi katika kuenea kwa UKIMWI. Aliamini kwamba ilikuwa vigumu kwa vijana waliofundwa kikamilifu katika majando, kuingia kwenye uasherati kwa urahisi. Aliwachukulia vijana wa Kimasai kama mfano mzuri, kwani kiwango cha ugonjwa huo kwa Wamasai kilikuwa kidogo sana (uk. 50).

Hoja ya Dkt. Hans katika nukuu hii kwamba sababu za kiutamaduni zilichangia katika kuenea kwa UKIMWI ina mashiko, kwani tohara ni suala la kiutamaduni. Anachoamini ni kuwa vijana waliopata mafunzo na kufanyiwa tohara wana maadili kuhusu maisha, tofauti na wale ambao hawajafanyiwa. Mfano unaohusu jamii ya Wamasai, unatoa picha ya namna wanavyodumisha utamaduni wao, likiwamo suala la tohara. Auvert na wenzake (2005) wanaeleza kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya tohara na kupungua kwa maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Nao, Gray na wenzake (2007), wanaunga mkono hoja hiyo kwamba tohara hupunguza uwezekano wa kupata magonjwa ya zinaa kama vile kaswende na kisonono, pamoja na saratani ya uume na maambukizi katika njia ya mkojo, hususani kwa watoto wachanga. Kwa mantiki hiyo, hoja kwamba tohara ni njia mojawapo ya kujikinga na magonjwa ina tija ya kitaaluma na kiafya na ina dhima kubwa kwa jamii. Kulingana na mtazamo wa Wanasosholojia ya Kifasihi kwamba, fasihi ni zao la

mipaka ya mabadiliko na mazingira ya jamii, ni wazi kuwa mhusika Omolo alihofia kuwa kitendo cha kuishi na govi ni kinyume na uhalisi wa maisha ya sasa na kingeweza kumsababishia kupata magonjwa. Uamuzi wa kulitoa govi hili ulitokana na kutafakari kwa kina athari za kuishi katika hali hiyo.

**Kujenga Ujasiri na Ukakamavu**

Tohara kwa kijana anayeingia katika utu uzima katika jamii za Kiafrika ina tija ya kumfanya awe jasiri na mkakamavu. BAKITA (2017) linaeleza kwamba ujasiri ni uwezo wa kukabiliana na jambo bila woga. Ujasiri huo hujengwa kutokana na mafunzo yanatolewa wakati wa tohara pamoja na mchakato mzima wa kuondoa govi. Nayo TUKI (2014) inasema, ukakamavu ni hali ya kustahimili mambo, yaani hali ya kutokubali kushindwa jambo kwa urahisi. Kijana anapokwenda kufanyiwa tohara hujengewa misingi ya kuwa na ukakamavu katika kukabiliana na matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii yake. Kimsingi, tohara huambatana na mafunzo ya kijamii na kimaadili, ambapo kijana huandaliwa kutoka hali ya utoto na kuingizwa katika majukumu ya kiutu uzima. Katika riwaya teule, mwandishi anabainisha hili kupitia kwa mhusika Omolo anayedadisi kuhusu tohara huku ikihusishwa na kufanya ngono. Mwandishi anaeleza kwamba:

> Omolo alikaa kimya kwa muda mrefu. Hasira zilianza kupungua. Akatahiriwe ndipo afanye mapenzi? Alijua desturi ya kutahiri ilikuwa imejengeka katika makabila mengi. Baadhi yao walikihusisha kitendo cha kutahiri na ujasiri, hasa wale waliotahiri vijana waliokwisha kuwa wakubwa. Mtu hudhihirisha ujasiri wake kwa kustahimili maumivu ya tohara bila kuonyesha dalili zozote usoni (uk. 29).

Katika jamii za Kiafrika, tohara hufanywa na Ngariba kwa kutumia vifaa vya asili kama vile visu, bila kutumia ganzi. Tendo hilo huhitaji mhusika awe na ujasiri, ukakamavu, na uvumilivu wa hali ya juu, kwani huweza kumsababishia maumivu makali. Hii inatokana na ukweli kwamba tohara humwandaa mhusika kukabiliana na majukumu makubwa na mazito likiwamo suala la ngono na, hatimaye, kujenga familia. Ndiyo maana mhusika hulazimika kupata mafunzo mbalimbali kuhusu masuala ya ujasiri na ukakamavu. Katika kushadidia hili, Ndeti (1972) anabainisha kwamba katika jamii ya Wakamba, tohara haikuwa tu kitendo cha kiafya, bali ni shule ya kijamii iliyoandaa vijana kwa maisha ya ujasiri, uaminifu, na uwajibikaji. Hii ni kwa kuwa tohara huambatana na mafunzo ya kinidhamu, usiri, na ustahimilivu, na kumpa mhusika ukakamavu wa kupambana na changamoto za maisha (Mbiti, 1969). Hoja za wataalamu hawa zinaonesha kwamba tohara ina tija kubwa katika jamii, kwani hutumika kama chombo cha kijamii cha kuwaandaa vijana kuwa na ujasiri, wenye uwezo wa kukabiliana na hofu, maumivu, na majukumu makubwa ya kifamilia na kijamii.

Kutokana na umuhimu huo, Dkt. Hans anamshauri na kumhimiza Omolo akafanyiwe tohara ili awe tayari kuyakabili majukumu mbalimbali katika jamii. Anasema:

> Na hilo govi lazima liondolewe. Linakufanya ujione tofauti na pia usite kukubali mwanamke auone mwili wako. Linakupa dosari katika nafsi yako. Katahiriwe uanze mapenzi na mtu umpendaye. Nitampigia simu Dkt. Chale akupokee kesho asubuhi, akufanyie oparesheni ndogo ya tohara ya kawaida, ungeifanya tohara ya kimila inayokamilisha jando lote, lakini umechelewa. Siyo mbaya sana, mambo mengine tutaweza kushauriana. Wewe umekuwa rafiki yangu. Nitazidi kukurafiki kwa nguvu. Ukinikwepa nitakutafuta mji mzima. Kesho tukutane kwa Dkt. Chale asubuhi, saa nne. Halafu uache tabia ya kutaka kuelezea na kujengea hoja kila jambo, inakupa kiburi cha kutetea kilema chako. Haya, tuonane kesho, kwa heri…" (uk. 355 – 356).

Katika nukuu hiyo, Dkt. Hans pamoja na mambo mengine, anakerwa na kitendo cha Omolo kuwa hajafanyiwa tohara hadi umri wake wa utu uzima. Anabainisha kwamba hii ndiyo sababu ya Omolo kuwaogopa wanawake na kushindwa kutimiza majukumu ya kifamilia. Anamhimiza akatahiriwe ili aweze kuvuka kutoka hali ya utoto kuwa mtu mzima na kuwa tayari kukabiliana na majukumu yanayofanywa na watu wazima, yaani kufanya ngono na kubeba majukumu ya kifamilia. Akitolea mfano kutoka jamii ya Wabukusi, Manguliechi (2007) anaeleza kwamba tohara katika jamii hiyo ni miongoni mwa sherehe muhimu sana, ambazo huwatoa vijana utotoni hadi utu uzima. Anafafanua zaidi kwamba sherehe ya tohara katika jamii hiyo pia hutumiwa kupitisha mila, itikadi, imani, falsafa, hisia, maadili, na mihemko ya Wabukusi. Maelezo hayo yanaungwa mkono na Simiyu (2007) anayeeleza kwamba katika jamii ya Wabukusi tohara imepewa uzito mkubwa sana na kwamba wasiotahiriwa hudharauliwa na kuchukuliwa kama watoto hata kama wamezeeka kiumri. Anaongeza kwamba katika jamii hiyo, mtu anapofariki akiwa hajatahiriwa, licha ya kufikisha umri wa kutahiriwa, ngariba mstaafu huletwa ili amtahiri na hapo baadaye marehemu husahaulika kabisa kana kwamba hakuwahi kuishi. Anafafanua zaidi kwamba hata watoto wanaozaliwa, kamwe huwa hawapewi jina lake. Kwa mtazamo wa Dkt. Hans, mtu ambaye hajafanyiwa tohara, ni sawa na mtoto na anatakiwa kufanyiwa ili awe mtu mzima. Pia, anamlinganisha na mtu ambaye ni mlemavu anayepaswa kusaidiwa ili kuondokana na ulemavu wake. Kulingana na fikra za Wanasosholojia ya Kifashi, jambo hili ni halisi katika maisha ya Waafrika, kwani asiyetahiriwa huchukuliwa kama mwenye upungufu fulani katika maisha yake.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili kuhusu tija za tohara katika maisha ya Waafrika kwa kumrejelea mhusika Omolo kutoka riwaya ya *Ua la Faraja* (2004). Mjadala ulijikita katika kubainisha tija hizo kwa kufungamanisha na uhalisia wa jambo hilo katika jamii. Matokeo yameonesha kwamba, kufanya tohara ni jadi ya baadhi ya makabila katika jamii za Kiafrika. Maingiliano baini ya jamii za Kiafrika na za kigeni yamechochea na kuendeleza jadi hiyo, hususani tohara kwa vijana wa kiume. Imejadiliwa kwamba kitendo cha mhusika Omolo kupinga tohara kinawakilisha jamii zenye mtazamo kuwa tohara huharibu maumbile ya mwanadamu na ni kinyume na mapenzi ya Mwenyezi Mungu aliyeutengeneza mwili wa kila mwanadamu kwa ukamilifu wake. Hata hivyo, matokeo yameonesha kwamba Omolo anakubaliana na washauri wake, hatimaye kufanyiwa tohora. Anafikia uamuzi huo baada ya kupata maarifa ya kutosha kuhusu tija za tohara. Makala hii ilimakinikia tija nne; nazo ni: kudumisha mila, kuleta heshima kwa mhusika, kujikinga na magonjwa, na kujenga ujasiri na ukakamavu. Matokeo yanaonesha kwamba Omolo baada ya kufanyiwa tohora, alijiona ni mwenye ufahari na heshima katika jamii yake. Ujasiri na ukakamavu wake uliongezeka katika familia na hata kazini kwake. Mtazamo wa wanauhalisia ndio ulioongoza katika kujenga usuli na mjadala wa matokeo ya makala hii.

**Marejeleo**

Auvert, B., Taljaard, D., Lagarde, E., Sobngwi-Tambekou, J., Sitta, R., & Puren, A. (2005). Randomised, Controlled Intervention Trial of Male Circumcision for Reduction of HIV Infection Risk: The ANRS 1265 Trial. *PLoS Medicine, 2*(11).

BAKITA. (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers Ltd.

Coser, L. (1972). *Sociology through Literature: An Introductory Reader*. The University of California: Prentice-Hall.

Dunsmuir, W. D., & Gordon, E. M. (1999). The history of Circumcision. *BJU International*, 83(S1), 1-12.

Duwe, M. (2023). Sifa za Hofu katika Maisha ya Mwanadamu: Uchunguzi wa Mhusika Ngoma kutoka Riwaya ya *Ua la Faraja*. *Nuru ya Kiswahili*, 2(2), 74-102.
Eliud, M. Ntiba G. & Dorcas, M. (2022). Maudhui katika Nyimbo za Tohara Zilizodenguliwa na Nyimbo za Dini za Kiigembe katika Kuyafikia Maendeleo Endelevu kwa Waigembe. *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), 273-287.
Fuluge, A. (2021). Usawiri wa Mchakato wa Kujiua katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi: Ni Mwangwi wa Mtanziko wa Kijamii? (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu). Chuo Kikuu cha Dodoma.
Gennep, A. (1977). *The Rite of Passage*. Routledge and Kegan Paul.
Glicksberg, C. I. (1972*). Literature and Society*. Martinus Nijhoff.
Gray, R. H., Kigozi, G., Serwadda, D., Makumbi, F., Watya, S., Nalugoda, F., Kiwanuka, N., Moulton, L. H., Chaudhary, M. A., Chen, M. Z., Sewankambo, N. K., Wabwire-Mangen, F., Bacon, M. C., Williams, C. F., Opendi, P., Reynolds, S. J., Laeyendecker, O., Quinn, T. C., & Wawer, M. J. (2007). Male Circumcision for HIV Prevention in Men in Rakai, Uganda: A Randomised Trial. *The Lancet, 369*(9562), 657-666.
Kanake, A. K. (2001). Changes and Continuity in the Practice of Clito: A Case Study of the Tharaka of Meru East. M.A. Thesis, Kenyatta University.
Manguliechi, W. J. (2007). An Oral Interview at His Miruri Home on Zo" April 2007 on Bukusu Circumcision Songs and History.
Mbiti, J. S. (1969). *African religions and philosophy* (2nd ed.). East African Educational Publishers.
M'Imanyara, A. (1992). *The Restatement of the Bantu Origin and Meru History*. Longman.
Mkufya, W. E. (2004). *Ua la Faraja*. Magrove Publishers.
Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Educational Publishers.
Mutwiri, G. (2005). Mitazamo ya Utendakazi wa Nyiso katika Jamii ya Watigania (Tasinifu ya Shahada ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
Nandwa, J. A. (1976). *Oral Literature of the Abaluhya*. University of Nairobi Press.
Ndeti, K. (1972). *Elements of Akamba life*. East African Publishing House.
Simiyu, W. F. (2007). Nyiso za Wabukusu: Maudhui na Lugha (Tasinifu ya Shahada ya Uzamili). Ndaki ya Kenyatta.
TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.
WHO & UNAIDS. (2007). *Male Circumcision: Global Trends and Determinants of Prevalence, Safety and Acceptability*. WHO.